



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI



Simu No: +255 (26) 2966008
Fax No: +255 (26) 2966008
Tovuti: www.uyuide.go.tz
Email: ded@uyuide.go.tz
Unapojibu tafadhali taja

2Barabara ya Boma,
45282 Uyui,
S.L.P. 610,
TABORA.

KUMB. NA. TDC/A.30/98/89

TAREHE: 21 JUNI, 2024

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui anawatangazia waombaji wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Uyui kuleta maombi ya kujaza nafasi Sitini na Tano (65) za kazi kwa nafasi ya Wakusanya Ushuru kwa masharti ya Mkataba.

1. MKUSANYA USHURU – NAFASI 65

SIFA ZA MWOMBAJI

- i) Awe raia wa Tanzania
- ii) Awe na Cheti cha kuzaliwa.
- iii) Awe na Kitambulisho cha NIDA/Namba ya NIDA.
- iv) Maombi yote yaandikwe kwa mkono na yaambatishwe picha moja (passport size) sambamba na nakala za vyeti.
- v) Awe na Umri wa kuanzia miaka 18 hadi 40.
- vi) Awe na elimu ya Kidato cha nne na kuendelea.
- vii) Awe na Mdhamini mwenye kiasi cha fedha au mali isiyo hamishika yenye thamani ya kuanzia TZS 3,000,000.00 (millioni tatu) na zaidi. Dhamana ya fedha italazimika kuwasilishwa Halmashauri hati ya au nyaraka ya umiliki inayotambulika na iliyothibitishwa kisheria kuwa ni mali ya mtoa dhamana.
- viii) Awe hajawahi kupatikana na makosa ya jinai au kuhukumiwa kifungo jela katika Mahakama yoyote Tanzania.
- ix) Awe tayari kufanyia kazi katika Kata au Kijiji atakachopangiwa na Halmashauri.

- x) Mtu yeyote aliyewahi kufanya kazi za Halmashauri kasha kuisababishia hasara ya upotevu wa mapato au unadaiwa na Halmashauri, **HAIRUHUSIWI KUOMBA KAZI YA KUKUSANYA MAPATO.**

2. NAMNA YA KUOMBA

- a) Mwombaji aambatishe barua ya uthibitisho wa makazi kutoka kwa Mwenyekiti wa Kijiji na kuthibitishwa na Mtendaji wa kijiji.
- b) Maombi yaonyeshe anwani kamili ya makazi yaani kata, Kijiji na Kitongoji. Pamoja na Simu inayopatikana muda wote.
- c) Watakaokidhi Vigezo na Kuchaguliwa kwa ajili ya usaili watajulishwa.
- d) Awe na wadhimini watatu ambao ni wakazi wa Wilaya ya Uyui Pamoja na namba za simu zinazopatikana muda wote.

3. MAJUKUMU YA MKUSANYA MAPATO

- a) Kukusanya mapato ya Halmashauri kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato vilivyopo katika Wilaya ya Uyui kwa kutumia mashine ya Kielekroniki (POS).
- b) Kuwasilisha benki kupitia akaunti ya mapato ya Halmashauri makusanyo yote yaliyokusanywa ndani ya saa 24 katika siku za kazi au siku ya kazi ya wiki au baada ya sikukuu.
- c) Kutoa risiti za mashine ya kielekroniki (POS) kiasi sawa na fedha atakayolipa mlipaji.
- d) Kutunza vifaa vya kukusanyia mapato (POS, REJESTA, Vifaa vyote vya POS) na nyaraka za benki au Halmashauri zinazothibitisha uingizaji wa fedha benki.
- e) Kufanya uhakiki kila siku wa makusanyo ya siku na taarifa ya mashine ya kukusanyia mapato.
- f) Kuwasilisha Halmashauri mashine ya kukusanyia mapato (POS) kwa ajili ya Ukaguzi/ uchunguzi.
- g) Kufanya kazi nyingine zinazohusu mapato kadri atakavyoelekezwa na mwajiri.

4. MUDA WA AJIRA

- Ajira ya Mkataba itakuwa ya miezi sita kuanzia mwezi husika baada ya kujaza mkataba wa ajira.
- Atakuwa chini ya uangalizi wa Mtendaji wa Kata na Kijiji husika.
- Mkusanyaji ataongezewa mkataba kutokana na juhudi yake katika kukusanya mapato.

5. MALIPO YA MKUSANYA MAPATO:-

Waombaji watakaopata nafasi na kupewa mkataba watalipwa mshahara kutokana na makubaliano ya kimkataba kati ya Mwajiri na Mwajiriwa.

Maombi yote yatumwe kwa anwani iliyopo hapo chini:-

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Uyui,
S.L.P 610,
TABORA.

Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 27 Juni, 2024.



Leokadia G. Humera

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),
UYUI**